# حكم السحر والكهانة وما يتعلق بها

## سماحة الشيخ عبد اللّه بن عبد العزيز بن باز رحمه الله

قام بترجمته إلى السواحلية

## الدكتور عبد اللّه خير

# *Hukumu ya uisilamu kuhusu uchawi na ukuhani*


***MUANDISHI NI***

***SHEIKH ABDUL AZIZ BIN ABDILLAHI BIN BAAZI [ALLAH AMREHEMU]***

***KIMEFASIRIWA NA***

***DR.ABDALLAH A. KHERI [PhD]***



طبع على نفقة وصية خولة دخيل الجسار رحمها الله (دولة الكويت) بإشراف اتحاد علماء إفريقيا

**kimefasiriwa kwa gharama ya wasia wa Khawla Dakheel Al-Jassar MwenyeziMungu arehemu (nchi ya Kuwait) kwa usimamizi wa Umoja wa Wanavyuoni wa Africa**

2016/1437

بســـــم الله الرحمن الرحيـــــم

# حكم السحر والكهانة وما يتعلق بها

## HUKUMU YA UISILAMU KUHUSU UCHAWI NA UKUHANI

Sifa njema zote ni za Allah, na Swala na Salamu zimfikie Nabii ambaye ni mtume wa mwisho, hakuna nabii baada yake.

Kutokana na ongezeko la hivi karibuni la wanaodai mambo yasiyoweza kufanywa na mtu wa kawaida hasa wale wanaodai kutibu na kuponya maradhi kupitia uchawi na ukuhani, na vile vile kuenea kwao katika baadhi ya miji, na kufaidika kwao kwa kupitia watu wasio na maarifa au ambao wana uchache wa dini. Hivyo basi nimeonelea, iwe ni miongoni mwa nasiha kwa ajili ya Allah na kwa ajili ya waja wake nipate kubainisha hatari hii kubwa inayo ukabili Uisilamu na Waisilamu kwa ujumla, kupatikana waja ambao wanajikurubisha zaidi kwa asiye kuwa Allah aliyetukuka na vile vile kutokana na kupatikana waja wenye kukanusha amri ya Allah na amri ya mjumbe wake Muhammad swala na salamu zimfikie.[1]

Nikitegemea msaada wa Allah nasema yafuatayo, Kwa kauli moja ya wanavyuoni inakubalika mtu kujitibu. Hivyo basi Muislamu inampasa aende kwa daktari kwa ajili ya kutefuta matibabu tofauti tofauti ya maradhi mbalimbali kama vile ya tumbo, vidonda na hata maradhi ya viungo na kadhalika, ili mgonjwa apate kupimwa ugonjwa aliyonao na atibiwe kwa mujibu wa dawa zinazokubalika kisheria na kitiba. Kufanya hivyo ni miongoni mwa njia za kawaida wala haipingani na mtu kutegemea na kutawakali kwa Allah, hakika Allah ameleta maradhi na ameleta na dawa zake. Hivyo basi atafahamu anayetaka kufahamu na atakosa kufahamu asiyetaka kufahamu. Lakini inakupasa ufahamu ya kuwa Allah hajaleta matibabu kwa waja wake katika kitu kilicho haramishwa.

Haifai kwa mgonjwa yeyote kwenda kwa waganga au makuhani ambao wanajidai kujua mambo ya ghaib au mambo fiche ili apate kujua maradhi yake. Pia haifai kuwaamini watu hao kwa chochote watakacho kwambia kwani wao huwa wanasema kwa kubahatisha sio semi za uhakika. Au wanatumia majini kuwasaidia katika kufanikisha mambo yao ya kiuchwawi. Basi watu wenye Imani kama hizo hukumu yao ni ukafiri na upotevu hasa wanapodai elimu ya ghaib au elimu aliyoificha Allah. Na Imam Muslim amepokea katika kitabu chake Sahih Muslim ya kwamba Mjumbe wa Allah Rehema na Amani zimfikie kasema:

[1] - Makala haya yalichapishwa katika Juzu ya pili ya kitabu "Bayaan Ashiya alati yatakiy biha sharr al-sihri". Na vile vile yalichapiswha tena kwa ukamilifu katika jarida moja la utafiti wa kiisilam, na jarida lingine la Yemen. Makala yalipewa jina 'Risalatu fi Hukmi al-sihri wa al-kahanah'

*“Mwenye kwenda kwa mpiga mburuga [Bao] akamuuliza kitu chochote, basi mtu huyo hatokubaliwa swala zake kwa muda wa siku arubaini”* pia imepokewa na Abu Hureyra radhi za Allah ziwe juu yake, kutoka kwa mtume rehema na amani zimfikie amesema: "*mwenye kumuendea mganga na akaamini aliyoambiwa basi amekufuru maamrisho ya mtume rehema na amani zimfikie*".Imepokewa na Abu Daud, na imeandikwa katika vitabu vinne vya Hadith na kusahihiswa na Al-haakim. Hadithi hii imesahihishwa na Al-haakim kwenye riwaya nyingine Mtume wa Allah Rehema na Amani zimfikie amesema: "*mwenye kumuendea mchawi na akaamini aliyo ambiwa basi amekufuru maamrisho ya Mtume Muhammad rehema na amani zimfikie"*

Imepokewa pia kwa Imran mtoto wa Husween radhi za Allah zimfikie amesema, amesema mtume wa Allah swala na salamu zimfikie (SAW) *“Sikatika sisi yeyote mwenye kutabiri kwa kupitia ndege au kutabiriwa, kufanya ukuhani au kufanyiwa, kufanya uchawi au kufanyiwa, yeyote mwenye kwenda kwa kuhani akaamini atakayoambiwa basi amekufuru maamrisho ya Mtume Muhammad (Rehma na Amain zimfikie)* {Imepokewa na Al-Bazaar kwa riwaya mzuri.}

Hadith zote hizi takatifu zilizotangulia zinakataza na kutoa onyo kali kwenda kwa wapiga mburuga, makuhani, wachawi na wanaofanana na wao kuwauliza chochote na kuwaamini. Ni jukumu kwa viongozi walio na madaraka na walio na hikima, kuyakataza maovu haya hasa ya kwenda kwa makuhani na wapiga ramli pia ni jukumu la walio madarakani na walio na hekima kuwazuia wenye kujitefutia riziki kwa njia hizo na kuyapinga mambo hayo kwa nguvu kabisa, pia ni jukumu la viongozi hao kuwazuia wale wanaofunga safari kuwaendea washirikina hao.

Wala haifai kughurika na kuamini kwa baadhi ya wanayoyasema ya kweli wala kwa wingi wa watu wanaokuja kwao kutokana na kutoifahamu kwao haki, basi haifai kuwaigiza kwani Mtume (Rehma na Amani zimfikie) alikataza kwenda kwao na kuwauliza maswali na hata kuwaamini kwa sababu ndani yake kuamini huko kuna uovu mkubwa na hatari na mwisho wake maangamivu kwa sababu wenye kufanya hayo ni waongo na ni madhalimu.

Hadith zilizotangulia ni dalili ya wazi ya kuwa wanayoyafanya makuhani na wachawi ni ukafiri, kwa sababu wanadai kujuwa mambo ya ghaib au mambo fiche na huo ni ukafiri.Inapasa kujua ya kwamba wote wawili, makuhani na wachawi wanawatumia majini na kumuabudu asiyekuwa Allah na huo ni ukafiri ulio wazi na ushirikina wa kumshirikisha Allah, yeyote katika viumbe atakaodai kujua eimu ya ghaibu aliyoificha Allah basi pia ni miongoni mwao, na yeyote mwenye kupambana na mambo hayo na akaamini basi yuko mbali na mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) (S.A.W).

Haifai kwa Muisilamu kukubali au kuwa mnyenyekevu kwa wanayoyadai kuwa wanatibu magonjwa kwa kutumia matalasimu, au hirizi zilizofungwa kwa rasasi na

nyinginezo ambazo miongoni mwa uzushi wanayo yafanya, haya yote ni miongoi mwa mambo ya kikuhani na udanganyifu kwa watu. Yeyote ambaye atakubali kufanyiwa hayo basi atakuwa amewasaidia katika upotofu na ukafiri wao.

Vile vile haipasi na ni haramu kwa muisilamu kwenda kuwauliza watu hao mke gani atamuozesha kijana wake, au jamaa yake, au kuuliza kuhusu siri za familia ya mume na mkewe kuhusu mapenzi yao, kutendeana uzuri au ubaya au hata kuwatenganisha kati yao na mengine mfano wa hayo yote hayafai kwa sababu haya ni miongoni mwa mambo ya ghaib ambayo hayajulikani na mtu yeyote isipokuwa Allah (SW). Kwa mujibu wa Qur’an, uchawi ni miongoni ya mambo ya kikafiri kama alivyosema Allah (sw) kuhusu wale Malaika wawili, Allah asema:

﴿ وَاتَّبَعُواْ مَا تَتْلُواْ الشَّيَاطِينُ عَلَى مُلْكِ سُلَيْمَانَ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَكِنَّ الشَّيْاطِينَ كَفَرُواْ يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنزِلَ عَلَى الْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَارُوتَ وَمَارُوتَ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولاَ إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلاَ تَكْفُرْ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ وَمَا هُم بِضَآرِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلاَّ بِإِذْنِ اللّهِ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلاَ يَنفَعُهُمْ وَلَقَدْ عَلِمُواْ لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الآخِرَةِ مِنْ خَلاَقٍ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْاْ بِهِ أَنفُسَهُمْ لَوْ كَانُواْ يَعْلَمُونَ ﴾ سورة البقرة الآية **102**.

*"Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru. Wakajifunza kwa hao wawili yale ya kumfarikisha mtu na mkewe. Wala hawawezi kumdhuru mtu ila kwa kutaka Mwenyezi Mungu. Na wanajifunza yatayowadhuru wala hayawanufaishi. Na hakika wanajua kwamba aliye khiari haya hatakuwa na fungu lolote katika Akhera. Na hakika ni kiovu mno walichojiuzia nafsi zao laiti wangelijua".*

Kwa mujibu wa aya hizi takatifu ziliotajwa, zinatufunza ya kwamba uchawi ni ukafiri, na kwamba wachawi kazi yao ni kufarikisha baina ya mume na mkewe. Vile vile aya zimetufunza ya kwamba uchawi haumdhuru wala kumnufaisha mtu ila kwa idhini ya Allah mwenye uwezo, kwa sababu Allah ndiye aliye muumba wa kheri na shari. Kwa hakika yamekuwa makubwa madhara, na yamekithiri mazungumzo kuwahusu hao wazushi ambao wamerithi elimu hizi za kiuganga na upotofu kutoka kwa washirikina na wakawachanganya mawazo walio na akili dhaifu ya kufahamu mambo. Basi sote tumetoka kwake na kwake yeye Allah tutarudi na yeye ndiye mwenye kutegemewa yaani Allah (SW). Aya pia imetufunza ya kuwa wale wanao jifunza uchawi, lengo huwa ni kujua mambo ambayo yatawadhuru, wala hawanufaiki na kitu chochote, na hawatakuwa na thamani yoyote mbele ya Allah.

Hili ni onyo kali kutoka kwa Allah na inatuonyesha uzito wa khasara watakayoipata hapa duniani na kesho akhira siku ya kiyama, hakika wameziuza nafsi

zao kwa thamani duni kabisa. Kwa ajili hiyo Allah amewashambulia sana katika Qur'an pale anaposema:

*Na hakika ni kiovu mno walichojiuzia* .([2]) ﴿ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْاْ بِهِ أَنفُسَهُمْ لَوْ كَانُواْ يَعْلَمُونَ

*nafsi zao laiti wangelijua.*

Neno hili (**شراء**) liliopo ndani ya aya maana yake ni biashara.

Basi tunamuomba Allah atupe salama na afiya na atuepushe na shari za wachawi na makuhani na wengineo wanaodai kuwa wanaufahamu wa mambo ya ghaib aliyoyaficha Allah. Vile vile tunamuomba Allah awahifadhi waisilamu na shari zao, na awawezeshe viongozi wa kiisilamu kujilinda nao na kutekeleza hukumu ya Allah juu yao mpaka wahifadhike waja kutokana na shari zao, madhara na vitendo vyao vibaya, kwani yeye ni mkwasi na ni mkarimu.

Hakika Allah (SW) amewawekea waja wake sheria na mambo ambayo wanaweza kujilinda na shari za wachawi kabla hazijawafikia. Kisha akawawekea na matibabu ambayo wanaweza kujitibu nayo pindi zikitokea shari za wachawi hao kwa rehema zake na ihsani yake katika kuwatimizia neema zake waja wake.

Yanayofuata ni maelezo na vitu ambavyo mtu anaweza kutumiya kujilinda na uchawi kabla haujatokea na baada ya kutokea katika mambo ambayo yameidhinishwa na Allah.

Ama dawa ya kujilinda na khatari ya uchawi kabla ya kukufikia, sinyengine inayofaa zaidi ila ni kutumia adhkari za kisheria zilizokubalika. Pamoja na duwa na kutumia kinga za duwa zilizothubutu katika mafundisho ya Bwana Mtume (SAW). Miongoni mwazo ni kusoma Ayatu Al-kursi baada ya kila swala ya faradhi, hasa baada ya zile dhikri zilizo thubutu kwa sharia baada ya swala ya faradhi.[3] Na vile vile kusoma Ayatul Al-kursi kabla ya kulala, nayo ni miongoni mwa Aya kubwa kabisa katika Qur'an aya yenyewe kama alivyosema Allah:

**﴿ اللهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّوْمُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِيْ يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلاَّ بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيْهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلاَ يُحِيْطُوْنَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلاَّ بِمَا شَاءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضَ وَلاَ يَئُوْدُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيْمُ. ﴾ (4)**

---

[2] - سورة البقرة، الآية 102.

[3] - "Subhanallah" mara 33, "Alhamdulillahi" mara 33 na "Allahuakbar" mara 33 "walailaha illa Allahu wahdahuu la sharika lahuu" mara 1, zote itkuwa ni mara 100

[4] - سورة البقرة ، الآية 255.

*Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni vyake pekee vyote vilivyomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala wao hawajui chochote katika vilio katika ujuzi wake, ila kwa atakalo mwenyewe. Enzi yake imetanda mbinguni na duniani; na wala haemewi na kuvilinda hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu.*

Miongoni mwa kinga zingine katika Qur'an ni kusoma:

﴿ قُلْ هُوَ اللهُ أَحَدٌ ﴾ ([5]) ، ﴿ قُلْ أَعُوْذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ﴾ ([6]) ، ﴿ قُلْ أَعُوْذُ بِرَبِّ النَّاسِ﴾ ([7])

Utasoma sura hizi tatu mpaka mwisho baada ya kila swala ya faradhi, na utazisoma mara tatu tatu baada ya swala ya Al-fajri na baada ya swala ya Magharibi, utaongezea aya mbili za mwisho za Suratul Baqarah na utasoma mpaka mwisho wa sura aya zenyewe asema Allah.

﴿ آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ ۚ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّن رُّسُلِهِ ۚ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۖ غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴾ ([8]).

Hakika imepokewa kwenye riwaya sahihi kutoka kwa Mtune (SAW) akisema: *"Yule ambaye atasoma Ayatul Kursi usiku basi atabakia chini ya hifadhi ya Allah wala hatokurubiwa na shetani hadi kupambazuke"*

Vile vile imepokewa kutoka kwa Mtume (SAW) akisem: *"Yule ambae atasoma Aya mbili za mwisho za Sutatl- Baqarah, wakati wa usiku basi zimemtosha" Na maana ya neno 'zimemtosha' yaani zitamlinda na kila shari na Allah ndiye anayejua zaidi.*

Na miongoni mwa kinga ni kukithirisha kusema:

*"Najilinda na kila shari iliyoumbwa kupitia* "أَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقْ" *maneno ya Allah yaliyokamilika "*

Utaomba duwa hii, Usiku au mchana au unapoingia kwenye nyumba au ukiwa majangwani au hewani au hata baharini hayo yote yametokana na mafunzo ya Mtume (SAW) aliposema:

---

[5] - سورة الإخلاص ، الآية 1.

[6] - سورة الفلق، الآية 1.

[7] – سور الناس، الآية 1.

[8] - سورة البقرة ، الآية 285.

"من نزل منزلا فقال: أعوذ بكلمات الله التامات من شر ما خلق. لم يضره شيء حتى يرتحل من منزله ذلك".

*"Mwenye kushukia kwenye nyumba, kisha Akasema: "Najilinda kupitia maneno ya Allah aliyokamilika na kila shari aliyoiumba. Basi (mtu huyo)" hatodhurika na kitu chochote hadi pale atakapo ondoka kwenye nyumba kama hiyo"*

Miongoni mwa (duwa njema) asome Muisilamu, mwanzo wa mchana na mwanzo wa usiku (yaani baada ya alfajri na baada ya magharib) mara tatu ni:

"بسم الله الذي لا يضر مع اسمه شيء في االأرض ولا في السماء وهو السميع العليم"

*"Naanza kwa jina la Allah ambaye kwa jina lake hakidhuriki kitu chochote mbinguni wala ardhini na yeye ni msikizi na ni mwenye elimu."*

Imethubutu kuwa Bwana Mtume katilia mkazo duwa hii na kwamba ni miongoni mwa sababu za kusalimika na kila jambo baya. Kwa hivyo, duwa hizi na nyengine kama hizi ni miongoni mwa kinga zinazomkinga mtu na shari za waganga na shari zenginezo, hasa yule ambae atazishikilia kwa ukweli, na Imani na kwa kumtegemea Allah pamoja na kufungua moyo wake kwa yale ambayo duwa hizi zimefundisha. Vile vile (duwa hizi) ni miongoni mwa silaha kubwa za kuondoa uchawi baada ya mtu kurogwa yaani kufanyiwa uchawi. Yapasa mtu awe mnyenyekevu kwa Allah na kumuomba yeye pekee aliye tukuka amuondoshee madhara na amuondoshee maovu.

Na miongoni mwaduwa zilizothubutu kutoka kwa Mtume (SAW) zinazo ponya maradhi ya uchawi na mengineyo na mtume akiwasomeya Maswahabah zake kwa ajili ya tiba ni:

"اللهم رب الناس اذهب البأس، واشف أنت الشافي لاشفاء إلا شفاؤك ، شفاء لا يغادر سقما" يقولها ثلاثا.

*"Ewe Mola wa watu (nakuomba) uondoshe madhara, na uponye kwani wewe (pekee) ndiye mwenye kuponya wala hakuna tiba yenye kuponya ila tiba yako, tiba ambayo haibakishi magonjwa "*aiseme duwa hii mara tatu.

Na miongoni mwa duwa za tiba ya uchawi, ni duwa ambayo aliyoombewa yeye Mtume (SAW) na Jibril nayo ni:

"بسم الله أرقيك من كل شيء يؤذيك ومن شرّ كل نفس أو عين حاسد الله يشفيك بسم الله أرقيك" و ليكرر ثلاث مرات

*“Kwa Jina la Allah naanza kukutibu Na kila kitu chenye kukuudhi na kila Shari ya nafsi, au jicho la hasidi, Allah akuponye, Kwa jina la Allah nakutibu”* unarudia mara tatu.

Miongoni mwa tiba ya mtu aliyerogwa au kufanyiwa uchawi, nayo ni tiba inayofaa sana mwanmume aliyefungwa na akawa hawezi kumuingilia mkewe, basi atachukuwa majani saba mabichi ya mkunazi, ayasage, au ayaponde kisha ayatiye kwenye chombo (ndoo) kisha atiye ndani yake maji ambayo yatamtosha kuogea kisha ayasomee hayo maji (kabla ya kuogea ) Ayatul Kursi, Suratul al-kafiruna, Suratul-Ikhlas suratul- Alfalaq na Suratul Annas utaongezea kwenye kisomo chake pia zile aya za kuponya uchawi kama zifuatavyo hapa .

قال الله تعالى: ﴿ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ ۖ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ، فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ، فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانقَلَبُوا صَاغِرِينَ ﴾ ([9]).

Pia muathiriwa anaweza kusoma aya ziliopo kwenye suratu Yunus kama asemavyo Allah:

﴿ فَلَمَّا جَاءَ السَّحَرَةُ قَالَ لَهُم مُّوسَىٰ أَلْقُوا مَا أَنتُم مُّلْقُونَ، فَلَمَّا أَلْقَوْا قَالَ مُوسَىٰ مَا جِئْتُم بِهِ السِّحْرُ ۖ إِنَّ اللَّهَ سَيُبْطِلُهُ ۖ إِنَّ اللَّهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ، وَيُحِقُّ اللَّهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴾ ([10])

Muathiriwa atangeza Aya ziliopo kwenye Suratu Twaha kama anavyo sema Allah:

﴿ قَالُوا:يَا مُوْسَى إِمَّا أَنْ تُلقِيَ وَإِمَّا أَنْ نَكُوْنَ أَوَّلَ مَنْ أَلْقَى، قَالَ بَلْ أَلْقُوْا فَإِذَا حِبَالُهُمْ وَعِصِيُّهُمْ يُخَيَّلُ إِلَيْهِ مِن سِحْرِهِمْ أَنَّهَا تَسْعَى، فَأَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُّوسَى ، قُلْنَا لَا تَخَفْ إِنَّكَ أَنتَ الْأَعْلَى ، وَأَلْقِ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوا إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى ﴾ ([11]).

Baada ya kusomea aya hizo kwa maji, atakunywa matama matatu, na yaliyobaki ataogea. Kwa uwezo wa Allah (SW) ataondokewa na hayo magonjwa, iwapoataonelea aendelee kutumia maji hayo mara ya pili au zaidi basi pia ni sawa aweza kufanya hivyo.

Miongoni mwa tiba za maradhi ya (uchawi), ni kujua zile sehemu zilizozikwa vitu vya kiuchawi, iwapo ni ardhini au kwenye milima, basi kutolewa vitu hivyo

[9] - Suratul A’araf , 117 – 119.
[10] - Surat Yunus, Aya 79-82.
[11] - Suratu Twaha, Aya 65-69.

kutabatwilisha uchawi lakini kuna umuhimu kutumia njia za kusunni kutoa vitu hivyo.

Ama kutibu maradhi ya uchawi kupitia wachawi ambao wanatumia mashetani kwa kuchinja, au kupitia vitu vingine kama makafara ni haramu na haifai, kwani kufanya hivyo ni kufanya kazi za mashetani na ni miongoni mwa ushirikina mkubwa.

Kwa hivyo, inapasa kujihadhari na hayo, kama ambavyo haifai kujitibu kwa kupitia makuhani, wapiga mburuga na waganga kwa sababu hawamuamini Allah na wanasema uwongo na kudai kujua mambo ya ghaib yaliofichwa na Allah na kudanganya watu. Na Mtume (saw) amehadharisha sana watu wasiende kwa waganga na kuwauliza maswali na kuamini maneno yao.

Vile vile imepokewa kwenye riwaya sahihi kutoka kwa Mtume Muhammad (saw) kuwa ameulizwa kuhusu Al-nashrah[12]

Akajibu: *"Ni katika amali za Shetani."*[13] Imepokewa na Ahmad na Abu Daud kwa mapokezi mazuri. Neno (nashra) ni kumponya mtu aliyepatikana na uganga kwa uganga kama alivyo ilivyo pokewa kutoka kwa mtu kuwa ni mambo yaliyo kuwa yafanywa kabla ya Uislamu nao ni kumuomba mchawi kumtibu aliye fanyiwa uchawi au kutibu uganga kwa uganga.

Ama kutibu maradhi ya uchawi (sihri) kwa kutumia Qur'an na duwa za kisharia na vyombo vya kihalali hakuna makossa kama tulivyotangulia kuelezea hapo mwanzo. Wametangulia kuangazia hayo wanavyuoni wakubwa Allah awarehemu kama Al-allama Ibnu Al-Qaim na Sheikh Abdurahman ibn Hassan katika kitabu *'Fathul Majid.'*

Allah ndiye mwenyeuwezo, tunamuomba awaafikie waisilamu kuwa na uwezo wa kupambana na kila baya, na awahifadhiye dini yao na awape ujuzi kwayo na afya ya kupambana na kila linalo khalifu sharia (ya uislilam). Tunaomba swala na salamu zimfikie Mja wake na Mtue wake Muhammad na jamaa zake na Swahaba zake.

---

[12] Kutibu maradhi ya uchawi kupitia kwa wachawi yalikuwa ni mambo ya kijahiliya yasiokuwa ya Kiislamu.

[13] Imepokewa na Imam Ahmad na Abu Dauwd Kwa Isnadi Mzuri